



HALMASHAURI YA MANISPAA YA SHINYANGA

Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa, Mtaazwa Chamagaha, S.L.P. 28, Shinyanga.

Simu: 026 2763213, Barua pepe: md@shinyangamc.go.tz, tovuti: www.shinyangamc.go.tz

Unapojibutafadhali taja:

Kumb. Na. SHY/MC/S.20/2 VOLX/56

Tarehe: 14 Juni, 2022

YAH: KURUDIA TANGAZO LA NAFASI YA KAZI

Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga imepata idhini ya utekelezaji wa Ajira Mpya kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Kupitia barua yenye Kumb Na. FA.97/228/01/9 ya Tarehe 13 Mei, 2021 kutoka kwa Katibu Mkuu Utumishi Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Mkurugenzi wa Manispaa ya Shinyanga anawatangazia wananchi wenye sifa na nia ya kufanya kazi katika Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga, kuomba nafasi ifuatayo kuanzia tarehe 14 Juni, 2022.

KATIBU MAHSUSI III NAFASI TATU (03)

SIFA ZA MWOMBAJI

- (i) Awe na cheti cha kuhitimu na kufaulu Kidato cha Nne (IV)
- (ii) Awe na amehudhuria mafunzo ya Uhazili na kufaulu mtihani wa Hatua ya Tatu.
- (iii) Awe amefaulu somo la Hatimkato ya Kiswahili na Kiingereza maneno 80 kwa dakika moja.
- (iv) Awe amepata mafunzo ya Kompyuta kutoka chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali na kupata cheti katika programu za Windows, Microsoft Office, Internet, E-mail na Publisher.
- (v) Awe raia wa Tanzania mwadilifu na mwenye umri kati ya miaka 18 hadi 45.

MAJUKUMU YA KAZI

- (i) Kuchapa barua, taarifa na nyaraka za kawaida.
- (ii) Kusaidia kupokea wageni na kuwasaili shida zao, na kuwaelekeza sehemu wanapoweza kushughulikiwa.
- (iii) Kusaidia kutunza taarifa/Kumbukumbu za matukio, miradi, wageni, tarehe za vikao, safari za Mkuu wake na ratiba ya kazi zingine zilizopangwa kutekelezwa katika Ofisi anamofanyia kazi, na kumuarifu Mkuu wake kwa wakati unaohitajika.
- (iv) Kusaidia kutafuta na kumpatia Mkuu wake majalada, nyaraka au kitu chochote kinachohitajika katika shughuli za kazi hapo ofisini.
- (v) Kusaidia kufikisha maelekezo ya Mkuu wake wa kazi kwa wasaidizi wake na pia kumuarifu kuhusu taarifa zozote anazokuwa amepewa na wasaidizi hao.
- (vi) Kusaidia kupokea majalada, kuyagawa kwa Maofisi walio katika sehemu alipo, na kuyakusanya, kuyatunza na kuyarudisha sehemu zinazohusika.
- (vii) Kutekeleza kazi zozote atakazokuwa amepangiwa na msimamizi wake wa kazi.

MSHAHARA:

Ngazi ya mshahara wa TGS B1

MASHARTI YA JUMLA YA MWOMBAJI KAZI

- (i) Awe Raia wa Tanzania mwenywe umri usiopungua miaka 18 hadi 45.
- (ii) Mwombaji aliyewahi kupatikana na kosa la jinai halitafikiwa.
- (iii) Aidha barua ya mwombaji ionyeshe anuani anayotumia kwa sasa pamoja na namba za simu ikiambatanishwa na:
 - (a) Maelezo binafsi ya mwombaji (CV).
 - (b) Nakala ya vyeti vya elimu na Taaluma
 - (c) Nakala ya cheti cha kuzaliwa.
- (iv) Weka picha mbili (2) za passport size za hivi karibuni.
- (v) Watakaoteuliwa kuhudhuria usaili (interview) watafahamishwa kupitia anuani na namba za simu walizotumia kwenye barua zao za maombi ya kazi.
- (vi) Testimonials na Provisional Results havitakubalika.
- (vii) Nakala zote za vyeti vya Shule, Chuo na cheti cha kuzaliwa zithibitishwe na Mwanasheria au Wakili yeyote aliyesajiliwa na kuthibitishwa.
- (x) Mwisho wa kupokea maombi haya ni tarehe 27/06/2022 siku ya Ijumaa saa 09:30 Alasiri

JINSI YA KUTUMA MAOMBI

Barua zote ziandikwe kwa mkono wa mwombaji nakutumwa kwa;

Mkurugenzi wa Manispaa,
Halmashauri ya Shinyanga,
S.L.P 28,
SHINYANGA.


MKURUGENZI WA MANISPAA
HALMASHAURI YA MANISPAA
SHINYANGA
Jomaary M. Satura
MKURUGENZI WA MANISPAA



Nakala: Katibu Tawala Mkoa,
Ofisi ya Mkuu wa Mkoa,
S.L.P 320.
SHINYANGA.

Katibu Tawala Wilaya,
Ofisi ya Mkuu wa Wilaya,
S.L.P 359.
SHINYANGA.